



**KARATASI
YA**

SHERIA YA MWAKA WA 2012 YA KUZUIA NA KUKOMESHA MATESO

UKWELI



Uganda iliidhinisha sheria ya kuzuia na kukomesha mateso katika kipengere cha 24 & 44 cha katiba ya mwaka wa 1995 inayowapa watu uhuru wa kutoteswa au kutendewa kinyama na kutopewa adhabu isivo va kiutu

Mateso ya kimwili ni pamoja na

- Kupigwa barabara, kugongwa kichwa, kupigwa ngumi, Mateke, kupigwa fimbo, kupigwa na matako ya bunduki, kurukia kwa tumbo;
- Kunyimwa chakula au kulazimishwa kula chakula kilichoharibika, kinyesi cha wanyama au cha binadamu;
- Kupigwa kwa kutumia umeme;
- Kuchoma kwa kutumia sigara, kuchoma kwa kutumia fimbo ya umeme, mafuta yenye kuchoma, asidi
- Kuzamisha kichwa cha mwathika ndani ya maji
- Kufungwa kamba au kulazimishwa kuweka mwili kwa sehemu inayofungwa na yenye kuleta wasiwasi;
- Ubakaji na utumiaji mbaya wa ngono ikiwa ni pamoja na kuingiza vitu vingine ndani ya sehemu za siri au kwa mkundu au mateso kwa kutumia umeme kwa sehemu za siri;
- Kukata sehemu za mwili
- Mateso ya meno au kutoa meno kwa nguvu;
- Kuwekwa kwa vitu vinavyoweza kuumiza kama mwanga wa jua na baridi nyingi, au
- Kutumia makaratasi ya plastiki ama vifaa vingine na kuyaweka kwa kichwa cha mwathirika kwa makusudi ya kumzuia kupata hewa safi.


Mateso ya kiakili au kisaikolojia ni pamoja na

- Kufunga kitambaa kwa macho;
- Kutisha mwathirika au mmoja wa familia yake kwa kutumia kifaa kinachoweza kuumiza mwili
- Mauaji au kitendo kingine kibaya;
- Kufungia mwathirika sehemu abapo ; hawezi kuwasiliana;
- Kufungia mwathirika peke yake ndani ya seli;
- Kuhoji mwathirika kwa mda mrefu na kumunyima wakati wake wa kawaida wa kulala au kupumzika;
- Kumtendea vibaya mmoja wa familia ya mwathirika
- Mwathirika kushuhudia mateso ya mmoja wa familia yake au jamii yake;

Mateso kuzidi kiasi ni nini?

Mtu anaweza kufungwa kifungo cha maisha akipatikana na hatia ya mateso kupita kiasi.

- Ikiwa mwenye mkosaji anatishia kutumia au kama alitumia siraha hatari
- Kama mkosaji ametumia ngono kama njia ya kutesa mtu
- Kama mwathirika alikuwa mtu mwenye ulemavu
- Kama mwathirika anapata mimba au alikuwa mjamzito
- Kama mkosaji anasababisha kifo
- Kama mwathirika aliwekwa kwa majaribiao ya kimadawa
- Kama mwathirika anapata ukimwi
- Kama mwathirika alikuwa chini ya umri wa myaka 18
- Kama mwathirika anapotesa uwezo wake wa kufanya kazi
- Kama kitendo cha mateso kinatendeka mara tena, au
- Mkosaji anatenda kitendo chochote ambacho mahakama inachukwa kuwa ni mateso kunita kiasi



Mateso ni nini chini ya sheria?

Mateso ni kitendo kinacho tendewa mtu kinacho sababisha maumivu kikikusudia kupata taarifa, kutoa adhabu, kutisha au kulazimisha mwathirika, kikitendwa na mtu yeyote awe ofisa wa uma au afisa yeyote au mtu binafsi ambaye anamadaraka.

Mateso ya kimadawa ni pamoja na

- Kumpa mtu madawa kwa nia ya kumletea kukubali au kupunguza uwezo wa akili
- Kutumia madawa ya kusababisha maumivu makali au alama za magonjwa Fulani na
- Aina nyingine za kukusudia kitendo kikali cha kinyama au adhabu isiyo ya kiutu.

Sheria inatoa adhabu gani kwa kitendo cha mateso?

- Mtu kupatikana na hatia ya mateso anapewa kifungo cha myaka 15 na /au kulipa faini ya shs za Uganda 7,200,000
- Mtu akipatikana na hatia ya kuwezesha au kusaidia kitendo cha mateso, kulipa pesa au kuagiza kitendo cha mateso anapewa kifungo cha myaka 7 na /au kulipa faini ya shs za Uganda 3,360,000

Je mtu binafsi anaweza kufungwa kwa ajiri ya kutenda kitendo cha mateso?

Siyo kama sheria ya kimataifa dhidi ya mateso, ofisa wa uma na maafisa wote wa serikali au binafsi wanaweza kufungwa kwa makosa ya mateso kwa mujibu wa sheria ya Uganda

Ni madawa gani yanayo patikana kwa ajiri ya waathirika na manusura wa mateso?

Fidia, ukarabati na aina yote ya malipo inayo amuriwa na serikali itapewa mwathirika/mtu aliyenusurika mateso

Hakutakuwa uhamisho wa mtu kwa nchi au sehemu inayodhaniwa kuwa kuna mateso

Taarifa yoyote inayotoka kwa mtu kupitia kwa mateso haitatumiwa kama ushahidi dhidi ya mtu huyo

**Sisi wote tunakazi ya kufanya kukomesha mateso!
Mtu yeyote pamoja na wewe unaweza kuripoti kesi ya mateso kwa polisi au kwa Tume ya haki za binadamu**

Serikali italinda mtu yeyote anayeripoti, anaye shuhudia na anaye lalamika kuhusu mateso

Mateso ni kitendo cha jinai. Hakun mpaka kuhusu mda ambao umepita kabla ya kuripoti kitendo hicho.

Kwa taarifa zaidi wasiriana na info@refugeelawproject.org au piga simu kwa 0776897057

